

Namna ya Kusoma na Kuelewa Jedwali Katika DHS

Jedwali zenye takwimu zinaweza kukutisha unapozitazama kwa mara ya kwanza. Kipeperushi hiki kimeandaliwa kukusaidia kusoma na kuelewa jedwali katika Utafiti wa Viashiria vya VVU/ UKIMWI na Malaria Tanzania (THMIS) 2011-12.

Mfano wa I. Ufahamu wa Njia za Kujikinga na VVU Ni swali lililoulizwa kwa kundi fulani la washiriki wa utafiti.

Hatua ya 1: Soma kichwa cha jedwali na kichwa kidogo cha jedwali. Vichwa hivi vya jedwali vitakufahamisha mada na kundi la washiriki linalozungumziwa. Jedwali hili, kwa mfano, linahusu ufahamu njia za kudhibiti maambukizi ya VVU miongoni mwa wanawake wenye miaka 15-49 nchini Tanzania.

Hatua ya 2: Pitia vichwa vya kolamu ya juu kutoka kushoto kwenda kulia. Hivi vinaelezea namna taarifa zilivyogawanywa katika makundi. Katika jedwali hili, kwa mfano, kila safu inawakilisha njia moja ya kuzuia maambukizi ya VVU. Safu ya mwisho inaonyesha idadi ya wanawake waliohojiwa.

Hatua ya 3: Soma vichwa vya safu – kolamu ya kwanza kutoka juu kwenda chini. Hivi vinaonyesha namna mbalimbali za mgawanyo wa takwimu katika makundi kwa kuzingatia tofauti baina ya washiriki. Katika jedwali hili, kwa mfano, tunaielezwa ufahamu wa wanawake wa njia za kujikinga na VVU kwa umri, ndoa, makazi – vijijini/mijini, Kanda wanayotokea, viwango vya elimu na utajiri. Majedwali mengi katika ripoti za DHS yatakuwa yamegawanywa katika makundi haya.

Hatua ya 4: Tazama safu ya mwisho chini ya jedwali. Asilimia hizi zinawakilisha jumla ya wanawake wote wenye miaka 15-49 wanaofahamu kila njia ya kuzuia maambukizi ya VVU. Katika jedwali hili, kwa mfano, 69.4% ya wanawake miaka 15-49 wanafahamu kwamba kutumia kondom kunapunguza hatari ya maambukizi ya VVU; na 83.8% wanafahamu kwamba kuwa na mpenzi mmoja tu asiye na maambukizi kunapunguza hatari ya maambukizi na 63.2% wanafahamu njia zote mbili za kuzuia maambukizi.

Hatua ya 5: Ili kuweza kufahamu ni asilimia ngapi ya wasichana (miaka 15-24) wanafahamu njia zote za kuzuia maambukizi ya VVU, chora mistari miwili ya kufikirika, kama inavyoonyeshwa katika jedwali. Hii inaonyesha kwamba 58.7% ya wasichana miaka 15-24 wanafahamu kwamba kutumia kondom na kuwa na mpenzi mmoja asiye na maambukizi kunapunguza hatari ya maambukizi ya VVU.

Table 4.2 Knowledge of HIV prevention methods

Percentage of women age 15-49 who, in response to prompted questions, say that people can reduce the risk of getting the AIDS virus by using condoms every time they have sexual intercourse, and by having one sex partner who is not infected and has no other partners, by background characteristics, Tanzania 2011-12

Background characteristic	Women			Number of women
	Percentage who say HIV can be prevented by:			
	Using condoms ¹	Limiting sexual intercourse to one uninfected partner ²	Using condoms and limiting sexual intercourse to one uninfected partner ^{1,2}	
Age				
15-24	65.1	79.9	58.7	4,303
15-19	59.4	76.4	52.9	2,414
20-24	72.3	84.5	66.1	1,888
25-29	74.3	86.9	69.1	1,902
30-39	73.2	87.1	67.5	2,932
40-49	68.3	84.4	60.9	1,831
Marital status				
Never married	64.9	81.6	59.3	2,798
Ever had sex	80.8	88.3	75.5	1,303
Never had sex	51.0	75.9	45.3	1,495
Married/living together	69.9	84.5	63.9	6,910
Divorced/separated/widowed	76.4	85.1	68.4	1,258
Residence				
Urban	78.2	92.6	74.7	2,956
Rural	66.1	80.6	59.0	8,011
Zone				
Eastern	81.0	93.7	78.5	1,696
Western	72.3	89.3	67.8	890
Southern	81.6	89.5	76.4	557
Southern Highlands	76.5	85.0	69.5	1,155
Southwest Highlands	55.0	72.5	46.6	1,101
Central	66.1	84.4	62.6	1,100
Northern	55.5	86.0	52.0	1,281
Lake	71.1	76.5	60.5	2,797
Education				
No education	52.4	71.0	44.4	1,955
Primary incomplete	64.0	78.7	55.9	1,380
Primary complete	74.1	86.2	68.1	5,713
Secondary+	76.4	93.3	73.4	1,919
Wealth quintile				
Lowest	58.2	74.6	50.7	1,864
Second	64.9	79.0	56.7	1,974
Middle	68.6	80.9	61.1	1,977
Fourth	72.7	85.5	66.3	2,257
Highest	77.6	93.7	74.9	2,895
Total	69.4	83.8	63.2	10,967

Fanya zoezi: Tumia jedwali hili kujibu maswali yafuatayo (majibu yako hapa chini – yamegeuzwa chini-juu):

- Ni asilimia ngapi ya wanawake walioolewa wanafahamu kwamba kutumia kondom ni kinga dhidi ya VVU?
- Ni wanawake wa Kanda gani wenye ufahamu mkubwa kwamba kuwa na mpenzi mmoja asiye na maambukizi kunapunguza hatari ya kuambukizwa VVU?
- Linganisha wanawake wasio na elimu na wale wenye elimu ya sekondari au zaidi. Kundi lipi linafahamu zaidi kuhusu njia za kujikinga na VVU?

kwa wanawake wenye elimu. ukinganisha na 71% tu ya wanawake wastokuwa na elimu. Ufahamu kuhusu kondom pia ni mkubwa zaidi fahamu kwamba kuwa na mpenzi mmoja asiye na maambukizi kunapunguza hatari ya kuambukizwa VVU - Mashariki—93.7% (b) Zaidi ya 90% ya wanawake wenye elimu ya sekondari au zaidi wana-

Mfano wa 2: Malipo kwa Ngono na Matumizi ya Kondom Swali Lililoulizwa kwa Kundi Fulani la Washiriki

Hatua ya 1: Soma kichwa cha jedwali na kichwa kidogo cha jedwali. Hapa, kwa mfano, jedwali linahusu malipo kwa ngono na matumizi ya kondom miongoni mwa wanaume miaka 15-49.

Hatua ya 2: Pitia vichwa vya kolamu—safu ya juu kutoka kushoto kwenda kulia. Katika mfano huu, kuna makundi mawili yanayoelezewa. Kundi la kwanza (a) ni asilimia ya wanaume waliolipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti kati ya wanaume wote waliohiriki katika utafiti. Kundi la pili (b) inahusu matumizi ya kondom walipojihusisha na ngono ya kulipia na inahusu wanaume ambao waliripoti kwamba wamewahi kulipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti tu.

Hatua ya 3: Tazama kundi la kwanza. Safu ya mwisho inaonyesha kwamba 8.5% ya wanaume wote walilipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti. Je, ni wanaume wangapi wanahusika katika kundi hili? 8,352 au wanaume wote katika utafiti?

Kundi la pili (b) inaulizwa, miongoni mwa wanaume waliolipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti, asilimia ngapi waliripoti kwamba walitumia kondom mara ya mwisho walipolipia ngono? Jibu ni 52.9%. Na ni wanaume wangapi wanahusika katika kundi hili? 708 tu, au 8.5% ya 8,352. Kundi la pili ni kundi dogo la kundi la kwanza.

Hatua ya 4: Katika baadhi ya kanda, hakuna wanaume wengi walioripoti kuwahi kulipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti. Kunapokuwa na matukio chini ya 25, takwimu hiyo itakuwa imewekewa alama ya nyota, kama unavyoona katika matumizi ya kondom mara ya mwisho ya kujamiiana miongoni mwa wanaume waliowahi kulipia ngono Mkoani Unguja na Pemba.

Kunapokuwa na matukio kati ya 25 na 49, takwimu hiyo inawekwa katika paradesi kumwonya msomaji kutumia takwimu husika kwa tahadhari, kwa mfano matumizi ya kondom mara ya mwisho ya kujamiiana miongoni mwa wanaume waliolipia ngono Nyanda za Juu Kusini na Nyanda za Juu Kusini Magharibi. Kwakuwa si wanaume wengi katika kanda hizi waliosema wamewahi kulipia ngono mwaka

Table 6.4 Payment for sexual intercourse and condom use at last paid sexual intercourse 1

Percentage of men age 15-49 who ever paid for sexual intercourse and percentage reporting payment for sexual intercourse in the past 12 months, and among them, the percentage reporting that a condom was used the last time they paid for sexual intercourse, by background characteristics, Tanzania 2011-12

Background characteristic	2 Among all men:		Among men who paid for sex in the past 12 months:	
	Percentage who paid for sexual intercourse in the past 12 months	Number of men	Percentage reporting condom use at last paid sexual intercourse	Number of men
Residence				
Urban	7.0	2,142	66.7	149
Rural	9.0	6,210	49.1	559
Mainland/Zanzibar				
Mainland	a 8.8	8,079	b 52.9	707
Urban	7.2	2,066	66.7	149
Rural	9.3	6,013	49.2	558
Zanzibar	0.3	273	*	1
Unguja	0.3	204	*	1
Pemba	0.5	69	*	0
Zone				
Eastern	5.9	1,363	4	63.2
Western	6.5	736	(60.5)	48
Southern	22.3	371	57.4	83
Southern Highlands	9.3	818	(64.4)	76
Southwest Highlands	4.9	851	(44.0)	41
Central	6.6	908	50.4	60
Northern	4.5	855	(57.0)	38
Lake	12.9	2,178	45.6	281
Middle	9.9	1,590	51.6	158
Fourth	8.9	1,749	53.0	156
Highest	5.6	2,123	63.3	119
Total	8.5	8,352	3 52.9	708

Note: Figures in parentheses are based on 25-49 unweighted cases. An asterisk indicates that a figure is based on fewer than 25 unweighted cases and has been suppressed.
nc = No cases



Note: When parentheses or asterisks are used in a table, the explanation will be noted under the table. If there are no parentheses or asterisks on a table, you can proceed with confidence that enough cases were included in all categories.

mmoja kabla ya utafiti, ni vigumu kupata takwimu sahihi kuhusu wanaume hao. Tumia takwimu hizi zilizoko katika paradesi kwa tahadhari.

Kumbuka: Paradesi au alama ya nyota zitakapotumika, ufafanuzi utatolewa chini ya jedwali husika. Ikiwa hakuna paradesi wala alama ya nyota katika jedwali, unaweza kuendelea kwa kujiamini kwamba kulikuwa na idadi ya kutosha katika kila kundi.

Kufahamu zaidi kuhusu idadi kabla na baada ya kufanyiwa marekebisho tazama mfano wa 4.

Zoezi: Tumia jedwali hili kujibu maswali yafuatayo (majibu yako hapa chini, yamegeuzwa chini-juu):

- Je, wapi kati ya Tanzania Bara na Zanzibar penye wanaume wengi zaidi waliokuwa wamelipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti?
- Je, ni kanda gani ambako wanaume wengi zaidi wameripoti kuwahi kulipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti?
- Katika maeneo ya mjini, ni asilimia ngapi ya wanaume waliolipia ngono mwaka mmoja uliopita walitumia kondom mara ya mwisho walipojiamiana?
- Ni asilimia ngapi ya wanaume Kanda ya Magharibi walitumia kondom mara ya mwisho walipojiamiana miongoni mwa wale walioripoti kuwahi kulipia ngono? Je, unaweza kuitumia takwimu hii kwa kujiamini?

a) Bara—8.8% ya wanaume walioripoti kuwahi kulipia ngono ukilinganisha na <1% Zanzibar; b) Kanda ya Kusini - 22.3%; c) 66.7%; d) 60.5%; lakini paradesi zinaonyesha kwamba takwimu hii inatokana na wanaume 25-49 tu walioripoti kuwahi kulipia ngono mwaka mmoja kabla ya utafiti, hivyo inapaswa itumike kwa tahadhari.

Mfano wa 3: Malaria kwa Watoto

Kulinganisha Takwimu na Kuelewa Mwenendo

Hatua ya 1: Soma kichwa cha jedwali na kichwa kidogo cha jedwali. Jedwali hili, kwa mfano, linahusu kiwango cha kuenea kwa malaria kwa watoto wenye miezi 6-59 kwa mujibu wa kipimo cha kawaida cha darubini.

Hatua ya 2: Pitia vichwa vya kolamu- mstari wa juu kutoka kushoto kwenda kulia. Katika jedwali hili, kwa mfano, kuna jambo moja tu linalozungumziwa, kiwango cha malaria kwa mujibu wa kipimo cha darubini.

Kolamu ya tatu, “idadi,” inaonyesha watoto wangapi walipimwa malaria katika utafiti. Katika jedwali hili, kwa mfano, jumla ya watoto 7,322 wenye miezi 6-59 walipimwa malaria.

Hatua ya 3: Pitia vichwa vya safu—kolamu ya kwanza kutoka juu kwenda chini. Hivi vinaonyesha namna mbalimbali za mgawanyo wa takwimu hizi katika makundi tofauti kutokana na tofauti za washiriki. Jedwali hili linawasilisha taarifa za malaria kwa watoto kwa umri wa mtoto, jinsi, makazi, mkoa, kiwango cha elimu cha mama, na kiwango cha utajiri katika kaya anayotoka. Takwimu katika makundi haya zitakusaidia kuelewa jinsi ambavyo viwango vya malaria vinatofautiana katika maeneo mbalimbali nchini.

Hatua ya 4: Miongoni mwa watoto wote, 4.1% ya watoto wenye miezi 6-59 nchini Tanzania walipopimwa walikutwa na malaria. Lakini idadi hii ni wastani wa kitaifa; haelezi jinsi ambavyo viwango vya malaria vinatofautiana maeneo mbalimbali ya nchi na baina ya makundi mbalimbali.

Jibu maswali yafuatayo ili uweze kuelewa jinsi viwango vya malaria vinavyotofautiana kwa makundi mbalimbali nchini:

- Nini kiwango cha chini na kiwango cha juu cha malaria katika mikoa nchini Tanzania? Kiwango cha malaria kinatofautiana kutoka kiwango cha chini 0.0% katika mikoa ya Arusha, Iringa, Mbeya, Singida, Rukwa, na baadhi ya maeneo ya Zanzibar hadi kiwango cha juu cha zaidi ya 20% Mkoani Geita.
- Angalia mwenendo: Je kiwango cha malaria kinaongezeka sambamba na umri? Kiwango cha elimu cha mama? Kiwango cha utajiri katika kaya?
- Linganisha makundi tofauti: Je, watoto wa kiume wana uwezekano mkubwa wa kuwa na malaria? Vipi kuhusu watoto waishio maeneo ya mijini?

Step 5: Je, hii ina umuhimu gani? Mameneja wa program wanaweza kutumia taarifa hizi kutengeneza mipango thabiti. Kwa mfano, baadhi ya mikoa haijaathiriwa sana na malaria, hivyo, kutenga fedha nyingi kwa ajili ya kudhibiti malaria katika mikoa hii inaweza kuwa ni matumizi mabaya ya fedha. Vivyo hivyo, kiwango cha malaria ni kikubwa zaidi miongoni mwa watoto wanaoishi katika familia maskini na miongoni mwa watoto ambao mama zao hawana elimu ya kutosha. Kuyafikia makundi haya yaliyo katika hatari kubwa zaidi linaweza kuwa ni jambo litakalozaa matunda katika kupambana na malaria.

Table 11.5 Prevalence of malaria in children 1		
Percentage of children age 6-59 months classified by microscopy as having malaria, by background characteristics, Tanzania 2011-12		
Background characteristic 3	Malaria prevalence according to microscopy 2	
	Malaria prevalence according to microscopy	Number of children tested
Age (in months)		
6-8	2.1	400
9-11	1.9	400
12-17	2.2	906
18-23	4.0	821
24-35	4.4	1,632
36-47	4.9	1,668
48-59	5.2	1,494
Sex		
Male	4.1	3,694
Female	4.1	3,628
Residence		
Urban	1.0	1,179
Rural	4.7	6,143
Region		
Dodoma	0.5	258
Arusha	0.0	225
Kilimanjaro	0.5	167
Tanga	2.5	405
Morogoro	6.9	242
Pwani	7.4	119
Dar es Salaam	0.3	379
Lindi	4.1	90
Mtwara	2.0	166
Ruvuma	0.8	403
Iringa	0.0	119
Mbeya	0.0	405
Singida	0.0	347
Tabora	3.8	363
Rukwa	0.0	179
Kigoma	9.9	296
Shinyanga	4.4	348
Kagera	5.5	408
Mwanza	5.4	419
Mara	14.4	392
Manyara	0.7	210
Njombe	1.4	167
Katavi	5.7	191
Simiyu	2.0	511
Geita	20.7	316
Kaskazini Unguja	0.0	24
Kusini Unguja	0.6	16
Mjini Magharibi	0.0	97
Kaskazini Pemba	0.0	30
Kusini Pemba	2.1	29
Mother's education²		
No education	6.1	1,647
Primary incomplete	5.2	876
Primary complete	3.3	3,555
Secondary+	1.5	536
Wealth quintile		
Lowest	5.3	1,722
Second	5.5	1,684
Middle	4.3	1,493
Fourth	3.6	1,304
Highest	0.6	1,119
Total	4.1	7,322

Mfano wa 4: Kuelewa Sampuli Katika Jedwali za DHS

Sampuli ni kundi la watu ambao wamechaguliwa kushiriki katika utafiti. Katika tafiti za DHS, sampuli inawakilisha wananchi wote. Nchi nyingi zinapendelea kukusanya taarifa na kuripoti kwa nchi nzima na pia kwa mikoa au kanda za nchi husika. Ili kufanya makadirio ya tofauti zilizopo katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa baadhi ya viashiria vya kidemografia, takwimu zilikusanywa kutoka katika mikoa yote 30 ya Tanzania.

Tafiti za DHS zimeandaliwa katika namna ambayo inafanikisha kupatikana kwa takwimu katika nchi na katika kila mkoa. Tunataka sampuli ya washiriki katika kila mkoa iendane na idadi halisi ya watu katika mkoa huo, na vivyo hivyo tunataka sampuli ya kitaifa iendane na idadi halisi ya watu nchini. Ikiwa mikoa katika nchi fulani inatofautiana kwa ukubwa na hasa ikiwa baadhi ya mikoa ina watu wachache sana, sampuli itakayochukuliwa bila kufuata utaratibu maalum inaweza isihusisha idadi ya kutosha ya watu kwa kila mojawapo ya mikoa kwa ajili ya kufanya tathmini.

Kwa mfano, ikiwa una fedha za kutosha kufanya mahojiano na wanawake 10,967 kwa utafiti ambao unapaswa kuwakilisha mikoa yote pamoja na nchi nzima (kama katika jedwali kulia). Nchini Tanzania, mikoa haijagawanywa kwa usawa: baadhi ya mikoa ina watu wengi (kwa mfano Dar es Salaam), wakati mikoa mingine ina watu wachache (kwa mfano, KusiniUnguja).

Mtakwimu anayendanda sampuli anaweza kufahamu wanawake wangapi wahojiwe katika kila mkoa ili kupata takwimu za uhakika. Kwa Tanzania, kwa mfano, kolamu yenye rangi ya bluu (1) inaonyesha idadi kamili ya wanawake waliochaguliwa na kuhojiwa kwa kila mkoa, ikitofautiana kutoka wanawake 277 Mkoani Dodoma hadi wanawake 629 Mkoani Dar es Salaam. Kwa idadi hizi, kuna washiriki wa kutosha kuweza kupata matokeo ya kuaminika katika kila mkoa, hata kwa mikoa yenye watu wachache.

Kwa mgawanyiko huu wa washiriki, baadhi ya mikoa imewakilishwa na watu wengi zaidi na baadhi imewakilishwa na watu wachache. Kwa mfano, idadi ya wakazi wa KusiniUnguja mwaka 2010 ilikuwa ni chini ya 1% ya watu wote nchini Tanzania. Kinyume chake, idadi ya wakazi wa Dar es Salaam ilikuwa ni karibu 10% ya watu wote Tanzania. Lakini kama kolamu ya bluu inavyoonyesha, utafiti wa DHS ulihoji wanawake 289 KusiniUnguja, au karibu 3% ya sampuli yote ya utafiti. Wakati huohuo, wanawake 629 tu ndio waliohojiwa kwa mkoa wa Dar es Salaam, karibu 6% ya sampuli nzima ya utafiti. Hii haiwakilishi kwa usahihi idadi ya watu nchini.

Ili kupata takwimu ambazo ni wakilishi kwa nchi nzima, mgawanyiko wa wanawake katika sampuli unapaswa kufanana na mgawanyiko wa wanawake nchini. Wanawake kutoka katika mikoa ambayo ni midogo, kama KusiniUnguja, wanapaswa kuwa wachache katika sampuli inayowakilisha wananchi wote. Vivyo hivyo, wanawake kutoka katika mikoa yenye watu wengi zaidi, kama Dar es Salaam, wanapaswa kuwa wengi zaidi. Kwa hiyo, wataalamu wa takwimu katika DHS kwa kutumia hesabu wamefanya marekebisho ya idadi ya wanawake katika kila mkoa ili uwakilishi wa kila mkoa katika jumla kuu kwa nchi nzima uweze kulingana. Idadi katika kolamu ya zambarau (2) zinawakilisha idadi iliyofanyiwa marekebisho. Jumla kuu ya wanawake katika sampuli 10,967 haijabadilika, lakini mgawanyiko wa idadi ya wanawake katika mikoa umebadilika ili kuwakilisha mchango wa kila mkoa katika jumla kuu ya wanawake nchi nzima.

Je, wataalam wa takwimu wanafanyaje marekebisho katika kila kundi? Wanahesabu upya makundi mbalimbali ili yafanane na idadi halisi katika nchi. Ukijaribu kulinganisha kolamu nyekundu (3) na idadi halisi ya watu nchini Tanzania, utaona kwamba wanawake katika kila mkoa wanawakilishwa kwa uzito sawa kama ulivyo uwakilishi wao katika jumla kuu nchi nzima. Idadi ya wanawake iliyorekebishwa KusiniUnguja imepungua, ili kuwakilisha idadi ndogo ya watu katika mkoa huo, wakati idadi iliyorekebishwa kwa mkoa wa Dar es Salaam imepanda kuwakilisha idadi kubwa ya watu katika mkoa huo.

Kwa kutengeneza sampuli na kuifanyia marekebisho, inawezekana kufanya mahojiano na idadi ya wanawake ya kutosha kuweza kupata takwimu za kuaminika kwa ngazi ya taifa na eneo husika pasipo kuvuruga mgawanyiko halisi wa watu nchini. Kwa ujumla, idadi iliyofanyiwa marekebisho ndiyo inayoonyeshwa katika kila jedwali la DHS, hivyo usiwe na wasiwasi ikiwa idadi hii itaonekana kuwa ndogo: inaweza kuwakilisha kwa usahihi idadi kubwa ya wanawake waliohojiwa. Kumbuka, kutakuwa na paradesi na alama ya nyota kuashiria kwamba idadi ilikuwa ndogo sana katika kundi fulani.

Table 3.1 Background characteristics of respondents

Percent distribution of women age 15-49 by selected background characteristics, Tanzania 2011-12

Background characteristic	Women		
	Weighted percent	Weighted number	Unweighted number
Region			
Dodoma	3.8	422	277
Arusha	3.0	331	341
Kilimanjaro	3.5	384	331
Tanga	5.2	566	352
Morogoro	3.6	399	341
Pwani	1.9	213	284
Dar es Salaam	9.9	1,084	629
Lindi	1.7	188	312
Mtwara	3.4	369	301
Ruvuma	6.2	684	364
Iringa	1.8	200	315
Mbeya	6.4	699	378
Singida	3.8	416	386
Tabora	3.9	432	440
Rukwa	1.7	187	342
Kigoma	4.2	458	417
Shinyanga	3.8	415	333
Kagera	4.1	448	340
Mwanza	5.2	570	430
Mara	4.0	433	441
Manyara	2.4	262	385
Njombe	2.5	271	317
Katawi	2.0	214	299
Simiyu	5.7	626	466
Geita	2.8	304	566
Kaskazini Unguja	0.4	42	319
Kusini Unguja	0.2	26	289
Mjini Magharibi	2.1	230	371
Kaskazini Pemba	0.4	47	300
Kusini Pemba	0.4	46	301
Total	100.0	10,967	10,967